

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA HABARI UTAMADUNI SANA NA MICHEZO

Simu: 026-2322129  
Nukushi: 026-2322128  
Baruapepe: km@habari.go.tz  
Tovuti: www. habari.go.tz



Jengo la LAPF,  
Ghorofa ya Nane,  
Makole Uhindini,  
S. L. P 25,  
DODOMA.

### TAARIFA KWA UMMA

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Harrison G. Mwakyembe (Mb), amekutana na msanii nyota wa Tanzania Nassibu Abdul Juma (Diamond) kwa lengo la kurejesha maelewano kwenye tasnia ya Sanaa ya Muziki nchini kufuatia hatua zinazochukuliwa na Wizara kuzuia baadhi ya kazi za Sanaa zinazoonekana kukiuka maadili ya nchi.

Kikao hicho kimefanyika katika Ofisi za Wizara Jijini Dar es Salaam, ambapo Dkt. Mwakyembe alifuatana na Naibu Waziri, Mhe. Juliana Shonza, Katibu Mtendaji wa BASATA, Bw. Godfrey Mwingereza na Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania, Bi. Joyce Fisoo, huku Diamond aliongozana na meneja wake watatu Bw. Sallam Sharaff, Bw. Hamis Taletale na Bw. Said Fella.

Dkt. Mwakyembe alisisitiza kuwa Serikali haina ugomvi wowote na wasanii nchini bali jukumu kubwa ni kusimamia maadili, na kukumbushia kauli ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere baada ya uhuru kwamba “Taifa lisilo na utamaduni wake ni sawa na Taifa mfu”, hivyo kuwaagiza watendaji wa Wizara na Taasisi zake ikiwemo BASATA, Bodi ya Filamu Tanzania na TCRA kukutana na makundi ya wasanii wa muziki kutoa elimu kuhusu taratibu za kuwasha kazi zao kwa mamlaka husika ili kujiridhisha na maudhui ya kazi hizo kabla ya kuzisambaza.

“Maamuzi ya kuzifungia baadhi ya nyimbo yanayafanywa kwa mujibu wa sheria na si kwa utashi binafsi wa kiongozi wa Wizara, hivyo basi ielevweke kwamba hatua zilizochukuliwa na Naibu Waziri Shonza hivi karibuni zilikuwa za Wizara kwa mujibu wa Sheria za nchi”, amesema Dkt. Mwakyembe.

Aidha Diamond alimhakikishia Dkt. Mwakyembe kuwa atashirikiana kwa karibu na Naibu Waziri Shonza pamoja na uongozi mzima wa Wizara katika kusimamia maadili ya kazi za sanaa, kwa kuwa mstari wa mbele katika kulinda utamaduni wa Tanzania.

Kwa upande wake Naibu Waziri Shonza alisisitiza umuhimu wa wasanii kufuata utaratibu kwa kuwasilisha kazi zao kwenye mamlaka husika ili kuepusha matatizo baadaye, na kufafanua kuwa suala la kulinda maadili ni endelevu. Pia amezitaka Bodi ya Filamu Tanzania na TCRA kukamilisha zoezi la kuonanisha kanuni za madaraja ya kazi za sanaa, ili kujua zile zinazofaa kuonekana na watu wazima peke yake zianze kuangaliwa kuanzia saa 6:00 usiku - saa 12:00 asubuhi.

Imetolewa Na:

Lorietha Laurence  
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.  
27/03/2018.